**102/3**
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**KARATASI 3**
**JULAI/AGOSTI, 2013**

**MUDA: SAA 2½**

| **102/3 Kiswahili P3 – Fasihi** |
| --- |
| Jumatano 11.00am –1.30 pm |
| 17/7/2013 (Awamu ya pili) |

**SHULE YA KITAIFA MARANDA**
**MTIHANI WA MWIGO**
**KIDATO CHA NNE, 2013**
**CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI (KENYA)**

## MAAGIZO

a) Jibu maswali **manne** pekee.
b) Swali la **kwanza** ni **lazima.**
c) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani : Riwaya, Tamthilia, Hadithi Fupi na Ushairi.
d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
e) **Karatasi hii ina kurasa 5 zilizopigwa chapa.**
f) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa maswali yote yamo na kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa.**
g) Kumbuka kuchora jedwali la maswali uliyoyajibu juu ya karatasi yako ya majibu.

## SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

1 a) Ngomezi ni nini ? (alama 2)

b) Eleza sifa **nne** za ngomezi. (alama 4)

c) Jadili dhima **tano** za ngomezi katika jamii yako. (alama 10)

d) Fafanua udhaifu wowote wa ngomezi. (alama 4)

## SEHEMU B: HADITHI FUPI

**Ken Walibora na Said A. Mohamed:** *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 2 au 3.*

2 " Nilithubutu kufanya jambo la ajabu sana katika maisha na hapo ndipo nimuombapo Mungu anisamehe."

a) Mzungumzaji alifanya jambo gani la ajabu ? Eleza ni kwa nini akalifanya jambo hilo la ajabu. (alama 4)

b) Eleza madhara yanayotokana na jambo alilolifanya mzungumzaji kwa jamii. (alama 6)

c) Toa mafunzo **matano** tunayoyapata kutokana na kisa linamotoka dondoo hili. (alama 10)

3 Eleza huku ukitoa mifano faafu ya mitindo ifuatayo ilivyotumika katika hadithi ulizopewa.

i) Ishara katika Gilasi ya Mwisho Makaburini. (alama 10)

ii) Balagha katika Shaka ya Mambo. (alama 10)

## SEHEMU C : RIWAYA

**Said A. Mohamed:** *Utengano*

*Jibu swali la 4 au 5.*

4 " Maonevu dhidi ya mwanamke ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii." Thibitisha. (alama 20)

5 "Lakini tamu isikulevye ukaisahau dunia. Dunia duara, ukicheza utachera!"

a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

b) Taja na utolee mifano ya tamathali za usemi **mbili** zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) 'Dunia duara, ukicheza utachera." Thibitisha utimilifu wa kauli hii kwa mujibu wa riwaya. (alama 12)

## SEHEMU D : USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7.*

6 *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**E. Kezilahabi :** *Mzee na Mzigo*

Piteni jamani, piteni haraka
Nendeni, nendeni huko mwendako
Mimi haraka, haraka sina
Mzigo wangu, mzigo mzito mno
Na chini sitaki kuuweka.

Vijana kwa nini hampiti?
Kwa nini mwanicheka kisogo?
**Mzigo** nilioubeba haupo kichwani
Lakini umenipinda mgongo na miguu
Na lazima nijiegemeze kichwani
Chini nendako.

Haya piteni! Piteni! Haraka ! Heei!
Mwafikiri mwaniacha nyuma
Njia ya maisha ni moja tu
Huko mwendako ndiko nilikotoka
Na nilipofikia wengine wenu
Hawatafika.

Kula nimekula na sasa mwasema
Niko nyuma ya wakati
Lakini kama mngepita mbele
Na uso wangu kuutazama
Ningewaambia **siri** ya miaka mingi.

**Maswali**

a) Eleza kilio cha mshairi huyu. (alama 2)

b) Onyesha tamathali za usemi **tatu** zilivyotumika katika shairi hili. (alama 6)

c) Fafanua hali-hisia ya shairi hili. (alama 3)

d) Eleza mbinu za kimuundo zilizotumika kulisarifu shairi hili. (alama 3)

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)

f) Kwa kurejelea shairi hili eleza maana ya: (alama 2)

i) Mzigo

ii) Siri

7 *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**Anguko la Jibwa**

Ndugu ona mbwa yule, ambaye **ananyekenya,**
Yaone mabuu yale, ambayo yamchezeya,
Kuwa leo yuafile, mwili yanautaniya,
Jana awile jasiri.

Juzi shujaa awile, pasiwe kumfikiya,
Kwenye makani yale, alipojisururiya,
Leo kuwa yuafile, mainzi yamchezeya,
Jana awile jasiri.

Mijino mikubwa ile, ambayo 'mejitokeya,
Yali kiwaliza wale, karibu walosogeya,
Tena akibweka yule, waoga walijinyiya,
Jana awile jasiri.

Kamwe kuishi milele , kupe ukijinyonyeya,
Walo chini yako wale, muhali unawaziya,
Ameshindwa yule pale, sembuse wewe sikiya,
Jana awile jasiri.

Kwa walo hai wale, yafaa kuzindukiya,
**Ni dunia maji male, muhimu kujiwaziya,**
Wazipunguze kelele, na kwingi kujishauya,
Jana awile jasiri.

**Maswali**

a) Eleza maana ya kiisitiari ya shairi hili. (alama 4)

b) Taja na ueleze aina za kishairi **mbili** katika shairi hili. (alama 4)

c) Kwa kutoa mifano mwafaka, taja aina **tatu** za uhuru wa kishairi zilizotumika katika shairi hili huku ukionyesha dhima zake. (alama 6)

d) Onyesha mtazamo wa mtunzi wa shairi hili. (alama 3)

d) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi.

i) Ni dunia maji male, muhimu kujiwaziya. (alama 2)

ii) Ananyekenya. (alama1)

## SEHEMU E: TAMTHILIA

**Timothy M. Arege :** *Mstahiki Meya*

*Jibu swali la 8 au 9.*

8 ' Nafikiri tuna mchango katika tatizo la uongozi wa Baraza. Sikuwahi kufikiri hivyo.'

a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b) Mzungumzaji na wenzake wana mchango gani katika tatizo la uongozi wa Baraza. (alama 8)

c) Fafanua athari **nne** za tatizo la uongozi wa Baraza kwa watu wa Cheneo. (alama 8)

9 Jadili mbinu **kumi** ambazo Mstahiki Meya alizitumia kuuendeleza uongozi wake wa kikandamizi dhidi ya raia wake. (alama 20)